**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAJI**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TABORA**

# MKATABA WA KUCHIMBA NA KUFUKIA MITARO KWA AJILI YA MIRADI YA MAJI KWA UFADHILI WA FEDHA ZA UVIKO-19

**KATI YA**

**Mamlaka ya Majisafi Na Usafi Wa Mazingira Tabora – TUWASA- (Mwajiri)**

**NA**

**Gereza La Uyui S.L.P 377 Tabora (Mtoa Huduma)**

**Februari, 2022**

## MKATABA WA UCHIMBAJI NA UFUKIAJI WA MITARO

1. Kwamba Mkataba huu ni wa huduma ya uchimbaji wa miferejí/mitaro, kulaza na kufukia bomba katika maeneo ya **Ulamba, Malolo-Mtakuja, Malolo-Mawiti, Malolo-Chang'ombe, Kidatu A-Radar, Kidatu B, Ikindwa na Kata ya Misha.**

2. Kwamba Mkataba huu unaanza tarehe__07__ Mwezi__03__ 2022 hadi tarehe__04__ Mwezi__06__2022. Mkataba huu utakamilika ndani ya miezi **Mitatu (3)** tangu tarehe ya kusaini Mkataba.

Kati ya

**Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (TUWASA) wa S.L.P.147 Tabora** [ambaye katika mkataba huu anafahamika *kama Mwajiri*], kwa upande mmoja,

Na

**Gereza la Uyui – Tabora S.L.P 377 Tabora** [ambaye katika mkataba huu anafahamika kama *Mtoa Huduma.]*

3. Kwamba, Mkataba huu ni ushuhuda wa pande zote mbili ambazo zinakubaliana kama ifuatavyo:-

3.1 Kwamba, mtoa huduma atatoa huduma ya uchimbaji wa mitaro, kulaza na kufukia mabomba katika maeneo ya **Ulamba, Malolo-Mtakuja, Malolo-Mawiti, Malolo-Chang'ombe, Kidatu A-Radar, Kidatu B, Ikindwa na Kata ya Misha** jumla ya urefu wa **Mita 42,055** ndani ya Manispaa ya Tabora kwa mchanganuo ufuatao-:

a. Ulamba Urefu wa Mita 3,700 @Tsh.1,000= 3,700,000
b. Malolo-Mtakuja Urefu wa Mita 3,567 @Tsh.1,000= 3,567,000
c. Malolo-Mawiti Urefu wa Mita 3,800 @Tsh.1,000= 3,800,000
d. Malolo-Chang'ombe Urefu wa Mita 1,168 @Tsh.1,000= 1,168,000
e. Kidatu "A"- Radar Mita 6,390 @Tsh.1,000= 6,390,000
f. Kidatu "B" Mita 12,560 @Tsh.1,000= 12,560,000
g. IKindwa Mita 2,270 @Tsh.1,000= 2,270,000
h. Kata ya Misha Mita 8,600 @Tsh.1,000= 8,600,000

3.2 Kwamba, mtoa huduma atachimba na kufukia mitaro yenye vipimo upana mita 0.5 na kina cha mita 0.9 kwa gharama ya **Tsh. 1000/=** kwa kila urefu wa mita moja kwa mabomba makubwa yenye vipenyo kuanzia inchi moja na nusu na kuendelea. Mitaro itakayo chimbwa itakaguliwa, kushuhudiwa na kisha kusainiwa nyaraka za uthibitisho wa kazi na pande zote mbili.

3.3 Kwamba, mtoa huduma katika kipindi chote cha mkataba huu atazingatia kikamilifu masuala yote ya kiafya na kiusalama wa kazi na watu wote wanaopaswa kuwa katika eneo la kazi katika hali ya mpango mzuri ili kuepusha hatari yoyote kwa watu hao na atazingatia mahitaji na kanuni zote za mazingira kama inavyoelekezwa na serikali ya Tanzania.

3.4 Kwamba, huduma zote na usanifu wa kazi vitakuwa vya aina na ubora kulingana na maelekezo ya mwajiri na vitaingizwa katika vipimo kama mwajiri anavyoainisha.

3.5 Kwamba, huduma zisizofuata makubaliano ya mkataba huu zitakataliwa na mwajiri na mtoa huduma kwa gharama zake mwenyewe atarekebisha au kutoa upya huduma iliyokataliwa hadi kumridhisha mwajiri.

3.6 Kwamba, kazi zingine zikijitokeza wakati wa utekelezaji wa kazi, mfano kusafisha njia kwa ajili ya kuchimba mtaro n.k, malipo yake yatajadiliwa na kukubaliwa na pande zote mbili.

3.7 Kwamba, katika tukio la hasara yoyote au uharibifu unaotokea katika utendaji wa aina yoyote wa nguvu za asili ambapo pande zote za mkataba kwa hali ya kawaida zisingeweza kutabili mapema, hasara au uharibifu kama huo utagharimiwa na mwajiri na mwajiriwa .

3.8 Mchanganuo wa Kazi

| | **Maelezo kuhusu kazi na Gharama** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **NA** | **KAZI** | **KIZIO** | **IDADI** | | **JUMLA** |
| 1 | Kuchimba na Kufukia Mtaro | M | 42,055 | 1,000 | 42,055,,000.00 |
| **JUMLA** | | | | | **42,055,000.00** |

4. Gharama ya kazi hii ni jumla ya Shilingi **MILIONI AROBAINI NA MBILI NA ELFU HAMSINI NA TANO TU (Tsh. 42,055,000.00).**

5. **Malipo**
   i. Patakuwa na malipo ya awali (*Advance* payment) ya **asilimia 30%** ya kiasi cha Mkataba huu ambayo ni kiasi cha Shilingi millioni kumi na mbili mia sita kumi na sita elfu mia tano tu (**Tsh. 12,616,500**) kwa ajili ya kumuwezesha Mtoa huduma aweze kuanza kazi hiyo.
   ii. Malipo yanayobaki ya **asilimia 70%** ya kiasi cha Mkataba huu ambayo ni sawa na kiasi cha Shilingi milioni ishirini na tisa mia nne thelatini na nane elfu mia tano tu (**Tsh. 29,438,500**) yatalipwa kwa kadri kazi itakavyokuwa inaendelea baada ya mtoa huduma kuwasilisha madai kwa kazi alizofanya.

6. Kama ushuhuda wa makubaliano pande zote mbili zimetia saini kwa namna Tarehe inavyosomeka hapo chini:

| **UPANDE WA MWAJIRI** *(TUWASA)* | **UPANDE WA MWAJIRIWA** *(UYUI MAGEREZA-TABORA)* |
|---|---|
| **Jina** Eng. Mayunga Kashilimu | **Jina** INSP Z. J YAMAKU |
| Cheo Kaimu Mkurugenzi Mtendaji | Cheo MWENYEKITI MIRADI |
| Sahihi [signature] | Sahihi [signature] |
| Tarehe 14/02/2022 | Tarehe 17.02.2022 |
| TUWASA S.L.P 147 TABORA | MKUU WA GEREZA KUU UYUI – TABORA |

MKUU WA GEREZA UYUI
Tarehe 17/02/2022
S.L.P. 9 TABORA